

## Maswali

1. Sulemani aliuliza Mungu nini?
2. Mungu alikubali matakwa ya Sulemani?
3. Sulemani angeuliza nini lakini hakuuliza?
4. Mbona hao wanawake walienda kwa Sulemani?
5. Mbona Sulemani alitaka upanga?
6. Hao wanawake wote wawili waliona uamuzi wa Sulemani ni mzuri?
7. Tunajifunza nini kwa hili somo?

## Majibu

1. Hekima.
2. Ndio.
3. Angeuliza mali au maisha marefu.
4. Kwa Sababu mtoto mmoja alikuwa amekufa.
5. Alitaka upanga ili akate mtoto kwa vipande viwili na ampe kila mmoja kipande kimoja.
6. La hasha, mwanamke mmoja aliona ni vyema lakini mama wa mtoto wa kweli hakutaka mtoto wake aumizwe.
7. Tunajifunza kwamba lazima tumuulize Mungu atusaidie na tutambue kwamba anasaidia.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



# 20 Hekima ya Sulemani

## Marejeo

1 Wafalme 3:16—18

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Sulemani alipata hekima kutoka kwa Mungu na akawa na uamuzi wa haki.


## Maneno maalum

1. Sulemani + ndoto + hekima.
2. Wanawake wawili + mtoto mmoja.
3. Sulemani + upanga.
4. Mama wa kweli + hekima

**20.1** Daudi alipokufa, mwanawe Sulemani akawa mfalme. Usiku moja alikuwa na ndoto. Kwa hiyo ndoto Mungu alimuahidi kumpa alichotaka. Sulemani akauliza, “Mpe mtumishi wako moyo wa kuelewa.” Aliuliza Mungu ampe hekima. Mungu alifurahi kwa ajili Sulemani hakuuliza mali au maisha marefu. Kwa hivyo hitaji lake lilikubaliwa.



**20.2** Siku moja wanawake wawili walimkujia hali mmoja amebeba kitoto mikononi, Akasema, “Oh Bwana wangu, sisi sote tunakaa nyumba moja na wote tulipata watoto. Mtoto wa huyu mama alikufa na akachukuwa wangu kwamba ni wake. Akisema wangu alikufa lakini sivyo, wake ndiye aliyekufa. Huyu mtoto ni wangu.” Mwingine akaseme, “Ia sivyo, mtoto ni wangu, aliyekufa ndiye wake.”



**20.3** Mfalme Sulemani alisema, “Kila mmoja anasema tofauti na mwingine.” Akageukia mtumishi wake na kusema, “Leta upanga.” Huyo akaleta upanga na akamwambia, “Kata vipande viwili na uawagawanyishie.” Ingawaje hakutaka kufanya hivyo, alitaka kujua mama wa kweli wa mtoto. Mpango wake ulifaulu. Mara moja, mwanamke mmoja aliruka na kulia, “Oh Bwana wangu, usifanye hivyo! Mpee huyu mtoto.” Lakini mwingine alikubaliana na Sulemani na akasema, “Usipeane mtoto kwa mmoja wetu, fanya vile umesema hiyo ni njia bora.”

**20.4** Hapo Sulemani akajua ni nani mwenye mtoto. Akasema, “Mpe mtoto mwanamke aliyesema kwanza.” Alijua mtoto ni wake kwa sababu aliona bora mtoto aende na huyo mwanamke mwingine kuliko kuona akikatwa vipande viwili. Alimpenda mtoto wake mpaka akaamua huyo mwanamke mwingine amchukue kuliko kuumizwa. Sulemani alijua kwamba huyu ni mama wake wa kweli – alimpenda mtoto wake sana. Sulemani alimruhusu aende ambebe mtoto wake. Kila mtu akamtambua Sulemani kwamba alikuwa mfalme mwenye hekima.

